


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



UTABIRI WA MVUA ZA MSIMU
(NOVEMBA, 2018 - APRILI, 2019)



Mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba, 2018 hadi Aprili, 2019).

Dondoo muhimu za mvua za *Msimu* (Novemba, 2018 – Aprili, 2019)

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mwelekeo wa mvua za *Msimu* kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua (kanda ya magharibi, kati, nyanda za juu kusini magharibi, kusini mwa nchi, ukanda wa pwani ya kusini pamoja na maeneo yaliyoko kusini mwa mkoa wa Morogoro) katika kipindi cha miezi ya Novemba, 2018 hadi Aprili, 2019. Aidha, taarifa hii inatoa mrejeo wa mvua za Vuli katika maeneo ya Ukanda wa Ziwa Victoria, pwani ya kaskazini na Nyanda za Juu Kaskazini-mashariki. Ushauri na tahadhari umetolewa kwa wadau wa sekta mbali mbali wanaotumia taarifa za hali ya hewa katika utekelezaji wa majukumu yao kama vile Kilimo na Usalama wa Chakula, Mifugo na Wanyamapori, Maliasili na Utalii, Uchukuzi na Mawasiliano, Nishati na Maji, Mamlaka za Miji, Afya pamoja na Menejimenti za Maafa. Muhtasari wa mwelekeo wa mvua hizo na athari zake ni kama ifuatavyo:

a) Mwelekeo wa mvua za *Msimu* kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka:

- (i) Mvua zinatarajiwa kuwa za juu ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi ya mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Mbeya, Njombe, Iringa, Ruvuma, kusini mwa mkoa wa Morogoro, Lindi na Mtwara. Kwa upande mwingine maeneo ya mikoa ya Kigoma, Katavi, Rukwa na Songwe yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani.
- (ii) Vipindi vingi vya mvua vinatarajiwa katika nusu ya kwanza ya msimu wa NDJFMA, 2018/19, nusu ya pili ya msimu mvua inatarajiwa kupungua.
- (iii) Mvua zinatarajiwa kuanza katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Novemba, 2018 katika mikoa ya Kigoma na Katavi na wiki ya tatu na ya nne katika maeneo mengine yaliyosalia. Mvua zinatarajiwa kuisha katika wiki ya nne ya mwezi Aprili, 2019 katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua.

b) Athari na ushauri

- (i) Matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza kupelekea maji kutuama na kusababisha mafuriko.
- (ii) Milipuko ya magonjwa inaweza kujitokeza hususan katika maeneo yenye miundombinu hafifu ya maji taka katika maeneo ya miji na maeneo yenye upungufu wa maji safi na salama.
- (iii) Hali ya unyevunyevu ardhini inatarajiwa kuwa ya kuridhisha katika maeneo mengi. Hata hivyo, vipindi vya ukavu, hususan katika mwezi Disemba, 2018 na Februari, 2019 vinaweza kusababisha kupungua kwa unyevunyevu ardhini hasa katika maeneo ya kati ya nchi.

I. MWELEKEO WA MVUA ZA MSIMU

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa inayotarajiwa (kama ilivyoelezwa katika kipengele II cha taarifa hii), mvua za juu ya wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka, maeneo yaliyosalia (Mikoa ya Kigoma, Katavi, Rukwa na Songwe) yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani. Hata hivyo, vipindi vingi vya mvua vinatarajiwa katika nusu ya kwanza ya msimu wa NDJFMA 2018/19 kutokana na uwezekano wa uwepeo wa upepo kutoka magharibi. Upepo huu unatarajiwa kubeba unyevunyevu kutoka misitu ya Kongo. Kipindi cha nusu ya pili cha msimu, mvua zinatarajiwa kupungua kutokana na joto la bahari sehemu ya kati ya bahari ya hindi kuendelea kuongezeka.

Mvua za *Msimu* ni mahususi katika maeneo ya magharibi mwa nchi, kanda ya kati, nyanda za juu kusini magharibi, kusini mwa nchi, ukanda wa pwani ya kusini pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro. Maeneo haya yanapata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka, unaoanza mwezi Novemba hadi Aprili ya mwaka unaofuata. Maelezo ya kina juu ya mwelekeo wa mvua hizo za msimu ni kama ifuatavyo:

i. Kanda ya Magharibi: (Mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi na Rukwa):

Katika kipindi cha NDJFMA 2018/19 mvua za juu ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika mkoa wa Tabora. Aidha, mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Kigoma, Katavi na Rukwa. Mvua hizi zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Novemba, 2018 katika mikoa ya Kigoma na Katavi, baadae kutawanyika katika mikoa ya Rukwa na Tabora ifikapo wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Novemba, 2018 na zinatarajiwa kuisha wiki ya nne ya mwezi Aprili, 2019.

ii. Kanda ya Kati: (Mikoa ya Singida na Dodoma):

Mvua katika maeneo haya zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Novemba, 2018. Maeneo haya yanatarajiwa kupata mvua za juu ya wastani hadi wastani katika kipindi cha NDJFMA 2018/19. Mvua zinatarajiwa kuisha kati ya wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Aprili, 2019.

iii. Nyanda za juu kusini magharibi na maeneo ya kusini mwa nchi (Mikoa ya Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe, Ruvuma pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro):


Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Novemba, 2018 na zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika maeneo mengi kwa kipindi cha NDJFMA, 2018/19.

Mvua zinatarajiwa kuisha kati ya wiki ya nne ya mwezi Aprili, 2019 na wiki ya kwanza ya mwezi Mei, 2019.

iv. Pwani ya kusini: (Mikoa ya Lindi na Mtwara):

Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Novemba, 2018 na zinatarajiwa kuwa za juu ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi katika kipindi cha miezi ya Novemba, 2018 hadi Januari, 2019.

Kipindi cha miezi ya Februari hadi Aprili, 2019 mvua zinatarajiwa kuwa za wastani katika maeneo mengi na zinatarajiwa kuisha katika wiki ya nne ya mwezi Aprili, 2019 na wiki ya kwanza ya mwezi Mei, 2019.



Ramani 1: Kushoto: Mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba, 2018 –Aprili, 2019) na Kulia: Wastani wa muda mrefu wa mvua za Msimu (1981 -2010).

Izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza kujitokeza hata katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani.

II. MIFUMO YA HALI YA HEWA

Hali ya joto la juu ya wastani inaonekana magharibi mwa Bahari ya Hindi na eneo la Ikweta la Bahari ya Pasifiki, joto katika eneo la Ikweta la Bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuendelea kuwepo katika kipindi cha Novemba, 2018 –Aprili, 2019. Kwa upande mwingine hali ya joto katika Bahari ya Hindi inatarajiwa kuongezeka. Joto zaidi linatarajiwa maeneo ya kati ya Bahari ya hindi na kuendelea kusambaa kuelekea eneo la mashariki. Pwani ya Somali inatarajiwa kuwa na joto la wastani hadi juu ya wastani.

Kwa upande mwingine eneo la Pwani ya Angola linatarajiwa kuwa na joto la chini ya wastani katika kipindi cha miezi ya Novemba, 2018 hadi Aprili, 2019.

Uwezekano wa kuwepo kwa vimbunga kusini magharibi mwa Bahari ya Hindi unatarajiwa kusababisha upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Kongo kuelekea nchini. Hali hii inatarajiwa kuongeza unyevunyevu katika baadhi ya maeneo ya nchi yanayopata msimu mmoja wa mvua.

III. ATHARI NA USHAURI

Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Wanyamapori

Katika kipindi cha mvua za 'Msimu' (Novemba hadi Aprili) 2018/19 hali ya unyevunyevu wa udongo kwa ustawi wa mazao na upatikanaji wa chakula cha samaki vinatarajiwa kuimarika katika maeneo mengi.

Hata hivyo, mazao yasiyohitaji maji mengi, kama vile mahindi, maharage na mtama, yanaweza kuathiriwa na hali ya unyevunyevu wa kupitiliza na maji kutuama. Aidha, magonjwa ya wanyama na uharibifu wa miundombinu ya kilimo na ile ya kufugia samaki vinaweza kujitokeza kutokana na mvua za juu ya wastani zinazotarajiwa katika maeneo hayo. Kwa upande mwingine, malisho na upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo na wanyama pori vinatarajiwa kuwa vya kuridhisha katika maeneo mengi.

Teknolojia ya uvunaji maji ya mvua iimarishwe ili kukidhi mahitaji ya maji katika kipindi cha baadae. Pamoja na ushauri huu watumiaji wa taarifa za hali ya hewa wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa wataalam wa sekta husika ikiwemo maafisa ugani.

Nishati, Madini na Maji

Kutokana mvua za juu ya wastani hadi wastani zinazotarajiwa katika maeneo mengi, ongezeko la maji katika mabwawa, mfano Mtera, itanufaika na ongezeko la maji kwa ajili ya uzalishaji wa umeme. Hata hivyo, sekta husika inashauriwa kuimarisha miundo mbinu ya usambazaji wa umeme ili kupunguza uwezekano wa athari zinazoweza kujitokeza.

Kwa upande wa sekta ya madini, wachimbaji, hususani wale wadogowadogo wanashauriwa kuwa makini kwani ongezeko la maji katika udongo linaweza kusababisha mmomonyoko wa ardhi au maji kujaa kwenye mashimo. Wataalam katika sekta ya madini wanashauriwa kuchukua hatua stahiki zikiwemo za kupunguza hasara kwa kuimarisha migodi

Upatikanaji wa maji kwa ajili ya umwagiliaji, matumizi ya nyumbani na uzalishaji umeme unatarajiwa kuwa mzuri; wakazi wa kandokando ya mito yenye historia ya kujaa na kuleta mafuriko wachukue tahadhari mapema wakishirikiana na taasisi husika za serikali na za kijamii.

Mamlaka za miji

Kutokana na vipindi vya mvua kubwa vinavyotarajiwa kujitokeza Mamlaka za miji na Jiji zinashauriwa kuchukua hatua stahiki kuhakikisha kuwa mifumo na njia za kupitisha maji zinafanya kazi katika kiwango cha kutosha ili kuepusha maji kutuama na kusababisha mafuriko na uharibifu wa miundombinu, upotevu wa maisha na mali.

Afya

Mvua za *Msimu* zinazotarajiwa zinaweza kusababisha milipuko ya magonjwa kama vile maleria, hivyo sekta ya Afya inashauriwa kuchukua hatua stahiki ikiwa pamoja na kutibu maji ya kunywa, kuzuia na kuharibu mazalia ya mbu, kudumisha usafi wa mazingira. Msisitizo unatolewa kwa Mamlaka husika kuhamasisha wananchi kuhusu ujenzi, uimarishaji na matumizi ya vyoo bora pamoja na matumizi ya vyandarua, madawa ya kinga na hatua nyingine stahiki ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

Menejimenti ya Maafa

Katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za juu ya wastani hadi wastani, inashauriwa taarifa zitolewe kwa wakazi wa maeneo ya mabondeni, karibu na mito, na yale ya tambarare, kupitia ngazi zinazohusika kama vile Makatibu Tawala na Kamati za maafa za Mkoa na Wilaya. Kamati zinashauriwa kufanyia maandalizi ikiwemo kutafuta rasilimali na kutenga bajeti za kukabiliana na maafa yanayoweza kujitokeza. Aidha, taasisi, kampuni za ujenzi na usafirishaji pamoja na wadau wengine wanashauriwa kujiandaa kuchukua hatua za dharura iwapo kutatokea uharibifu wa miundombinu ili kupunguza athari na hasara zinazoweza kutokea. Kwa upande mwingine, katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani, wananchi na wadau wengine wanashauriwa kuendelea na shughuli za kiuchumi na kijamii kama kawaida; hata hivyo, wanasisitizwa kujiandaa na madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na mvua hizi, hasa wale wanaokaa maeneo hatarishi.

Vyombo vya habari

Vyombo vya habari vinashauriwa kufuatilia, kupata na kusambaza taarifa sahihi za mienendo ya hali ya hewa kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na kutumia wataalam wa sekta husika katika kuandaa na kufikisha taarifa za masuala mtambuka ya hali ya hewa kwa jamii. Ni wajibu wa vyombo vya habari kutafuta na kutumia ushauri wa kisekta kutoka kwa watoa taarifa wa sekta mbalimbali zinazotumia taarifa za hali ya hewa ili kuujulisha umma athari za kisekta. Aidha, vyombo vya habari vinashauriwa kuandaa na kusambaza makala za kitaaluma zenye lengo la kuhabarisha jamii juu ya matumizi sahihi ya utabiri uliotolewa.

Mamlaka ya Hali ya hewa Tanzania (TMA) inawashauri watumiaji wote wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, mamlaka za wanyama pori, sekta za maji na afya kuendelea kufuatilia na kutumia ushauri wa kitaalam katika shughuli zao za kila siku.

Zingatio: Mwelekeo wa mvua uliotolewa hapa umezingatia zaidi kipindi cha msimu na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mabadiliko ya muda mfupi katika maeneo madogo utazingatiwa katika uchambuzi wa utabiri wa muda wa kati na mfupi. Watumiaji wa taarifa za utabiri huu wanashauriwa pia kufuatilia tabiri za saa 24, siku 10 pamoja na za mwezi kama zinavyotolewa na Mamlaka ya hali ya Hewa Tanzania.

IV. MREJEO WA MVUA ZA VULI, 2018

Mvua za Vuli zinazoendelea katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka zilianza mwezi Septemba, hususani katika maeneo machache ya Ukanda wa Ziwa Victoria na yale ya pwani ya Kaskazini. Mtawanyiko wa mvua hizi bado ni hafifu katika maeneo mengi. Kwa upande wa Nyanda za Juu Kaskazini-mashariki, mvua bado hazijaanza. Hali hii imetokana na joto la bahari kuendelea kuwa juu ya wastani katika pwani ya nchi ya Somalia na kupelekea unyevunyevu kuwa hafifu katika nchi yetu, hususani katika maeneo ya pwani ya Kaskazini na yale ya Nyanda za Juu Kaskazini-mashariki.

Mvua katika maeneo ya Ukanda wa Ziwa Victoria zinatarajiwa kuendelea vizuri katika kipindi kilichobakia cha msimu. Katika maeneo ya pwani ya Kaskazini, mtawanyiko wa mvua unatarajiwa kuanza kuimarika katika wiki ya nne ya mwezi Oktoba na kuendelea vizuri katika mwezi Novemba, 2018. Kwa upande wa Nyanda za Juu Kaskazini-mashariki, mvua zinatarajiwa kuanza kuelekea mwishoni mwa mwezi Oktoba na kuimarika katika mwezi Novemba, 2018. Hata hivyo, kuna uwezekano mkubwa wa kuwa na mvua chache katika mwezi Disemba, 2018 katika maeneo mengi ya pwani ya Kaskazini na Nyanda za Juu Kaskazini-mashariki. Hivyo wakulima wanaendelea kushauriwa kufuatilia utabiri wa siku kumi (10) na kupata ushauri kwa Maafisa Ugani.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa taarifa za mwelekeo wa mvua nchini kila inapobidi.

Imetolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania:

Dkt. Agnes L. Kijazi

MKURUGENZI MKUU

Imetolewa: 18 OKTOBA, 2018